

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: “UTUMISHI” D.S.M

Simu Na: +255 22 2118531/4

Nukushi: +255 22 2125299

Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: www.utumishi.go.tz



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S. L. P. 2483,
11404 DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) KUHAMIA MAKAO MAKUU YA NCHI- DODOMA

1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari nimewaita kuwajulisha kwamba safari ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kuhamia Dodoma inaanza rasmi leo. Kama mjuavyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka ahadi kwamba hadi kufikia Mwaka 2020, shughuli zote za Serikali zitakuwa zimehamishiwa Makao Makuu ya Serikali ambapo Wizara zote zitakuwa zimehamia Mjini Dodoma. Ahadi hii ilitolewa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Siku ya Mashujaa yaliyofanyika **tarehe 25 Julai, 2016**. Aidha, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) alitoa maelekezo na kuainisha utaratibu wa Wizara na Taasisi zote za Serikali kuhamia Makao Makuu ya Nchi huko Dodoma kwa Awamu Nne. Awamu ya Kwanza inayowahusu Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu na baadhi ya watumishi ikamilike ifikapo tarehe **28 Februari 2017**.

